
# Serikali ya Kilifi yazindua mpango maalumu wa kuwahudumia wananchi wa maeneo ya mashinani



**Mheshimiwa Gavana Gideon Mung'aro**

**Na MISHI ZIRO**

Mnamo Machi mwaka huu, serikali ya Kaunti ya Kilifi chini ya uongozi wa Gavana Gideon Mung'aro ilizindua mpango maalumu maarufu kama "Kaunti Mashinani" kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma bora kwa wakazi wa Kilifi.

Uzinduzi huo ulilenga kupeleka huduma za serikali ya Kaunti karibu na wananchi hasa wale wa vijijini ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakigharimika sana kutafuta nauli ili kusafiri hadi mijini kupata huduma za Kaunti kwa sababu ofisi nyingi ziko mijini.

Gavana Mung'aro, wakati wa uzinduzi rasmi wa mpango huo, alisema kuwa utakuwa 'kifungua-macho' kwake na utawala wake kuhusu kufuatilia hali halisi ya maendeleo katika maeneo ya mashinani.

"Mpango huu unalenga kuhakikisha kuwa maafisa wa serikali yangu kutoka vitengo mbalimbali wamejitolea kutekeleza majukumu waliotwikwa kulingana na vitengo vyao bila kuzembea.

Kama wewe ni afisa wa kilimo, utaenda nyanjani kuwatafuta watu ili uweze kuwafundisha kuhusu kilimo, lakini sio kukaa ofisini tu kwa starehe ilhali kazi yako ni ya kuenda nyanjani," alisema Bw Mung'aro.

Gavana, vilevile, alisema mpango huo wa huduma mashinani utawalazimu maafisa wote wakuu kutoka idara mbalimbali za Kaunti wakiwemo mawaziri na makatibu wao kutekeleza majukumu yao ya kikazi wakiwa mashinani kwa muda wa wiki mbili.

"Mpango huu utakuwa ukitekelezwa kila baada ya miezi minne ili kuimarisha utoaji huduma kwa wakati, na kuwezesha wakazi wa Kilifi kutangamana na viongozi wao ili kuwa na usemi kuhusu miradi tunayoipa kipaumbele," akasema Bw Mung'aro.

Katika kaunti-ndogo ya Magarini ambapo wakazi pia walinufaika kwa mpango huo, Gavana Mung'aro alitembelea eneo la Kadzandani, wadi ya Adu, ambako alikagua mradi wa maji na kushuhudia shughuli ya kuchimbwa kwa mabwawa 3 ya maji pamoja na kukagua visima kadhaa vya maji vilivyo katika eneo hilo ili kuhakikisha wakazi wa sehemu hiyo wanapata maji ya kunywa.

"Tumeambiwa kuwa katika muda wa wiki moja iliyopita, visima vyote hapa havikuwa vinafanya kazi, Mheshimiwa Diwani alisema anataka kuchimba visima vipya, lakini tumegundua visima vingi hapa vimejaa tope ndiyo maana maji hayakuwa yanapatikana. Ila sasa vimechimbwa upya na tayari maji yameanza kutoka," alisema Bw Mung'aro.

Aidha, mawaziri katika serikali ya kaunti hii pia walipongeza mpango huo wakisema umewapa fursa ya kufahamu changamoto za wananchi.

Mpango huo wa Kaunti Mashinani unatekelezwa katika maeneo-bunge yote saba ya Kaunti ya Kilifi ambapo Gavana aliwahakikishia wakulima kuwa serikali yake itaboresha sekta ya kilimo ili waweze kuzalisha chakula cha kutosha, kukabili tatizo la njaa ambalo limekuwa likishuhudiwa mara kwa mara katika Kaunti ya Kilifi.

Akizungumza katika eneo la Chonyi, Mung'aro alisema serikali ya Kaunti iko katika harakati ya kufanyia ukarabati matingatinga yaliyoharibika kwa ajili ya kusaidia shughuli za Kilimo.

"Nina ahidi, yale matingatinga yote ambayo tuliyapata yameachwa na serikali iliyopita yakiwa yameharibika, tutahakikisha tumeyarekebisha ili wakulima wasipate taabu ya kulimiwa mashamba yao.

Kwa sasa tumeweza kurekebisha matingatinga 22 ambapo mengine tumepeleka Magarini hapa Chonyi yatakuja mawili kesho," alisema Bw Mung'aro.

Mbali na hayo, Gavana amejaribu kufanya kila awezalo kuboresha miundomsingi kwa kuhakikisha wakazi wa Kilifi wanapata huduma bora za afya.

"Hili ni jambo ninalolipa kipaumbele ndiyo maana nimezunguka kaunti hii kila mahali. Mara nyingi mnaniona niko hospitalini hapa, mara niko katika ile nyingine, ili kuhakikisha watu wa Kilifi wamepata huduma bora za matibabu. Na hayo ndiyo maendeleo ambayo tunataka hapa Kilifi," alisema Bw Mung'aro.

Kaunti ya Kilifi ni miongoni mwa sehemu zinazokumbwa na tatizo la ardhi na kuchangia sana tatizo la uskwota.

Alipozuru ofisi za ardhi mjini Kilifi, Gavana Mung'aro alisema serikali yake itahakikisha uskwota unakabiliwa huku akiahidi kutoa hatimiliki za ardhi kwa wakazi ili waweze kuishi kwa amani bila kusumbuliwa na mtu yeyote.

"Kuna kitu kimoja ninataka kukimaliza, shida ya uskwota, tunataka tuwape hatimiliki, kama kesho tutawakuta Muyeye, siku nyingine Chakama ama Mida, tukiwa na utaratibu huu, itakua rahisi. Tunafaa kuwa na mfumo ambao utatambua mwenye hatimiliki mara tu unapoandika jina lake, hii itatuwezesha kudhibiti hali ya maskwota," aliongeza Bw Mung'aro.

Akiwa ziarani eneo la Ganze kuendeleza mpango huo, Gavana alitembelea miradi mbalimbali ikiwemo ofisi za Kaunti katika eneo-bunge ili kuboresha mazingira ya wafanyakazi wa serikali yake wanaohudumu katika eneo-bunge hilo.

Wananchi katika eneo hilo walimpongeza gavana huyo kwa kuanzisha mpango huo wakisema utawapa fursa ya kutangamana na viongozi wao.

Akiwa Ganze pia alitembelea zahanati ya Ganze, kituo cha kutoa mafunzo kwa vijana na kituo cha kibiashara.

Kiongozi huyo wa kaunti aliahidi kunyanyua hadhi ya taasisi za mafunzo ya ufundi katika kaunti (VTC).

Akiwa eneo la Bamba, Gavana Mung'aro alishuhudia utoaji hatimiliki ya ardhi kwa kikundi cha wakazi wa Mitangani cha "Mitangano Group Ranch" na kuahidi kumaliza utata wa ardhi unaowakumba wakazi wa eneo hilo.

"Shamba hili ambalo leo tunatoa hatimiliki zake lazima tulikatekate na tukabidhi kwa wananchi, ninajua kuna taabu sana na shamba hili la jamii, na mimi kati ya wabunge wote nikiwa bungeni nilikuwa mpinzani wa shamba hili kuandikiwa hatimiliki moja," alisema Bw Mung'aro.

Mpango huu wa kaunti mashinani ulibuniwa kwa malengo ya kukabiliana na tatizo la afya, maji, kilimo na kuangazia masuala ya vijana na wanawake.

Akiwa Kaloleni, Gavana aliangazia suala la afya hasa hospitali ya St Lukes.

"Tumekuja Kaloleni, ajenda ni moja ambayo imeleta Kaloleni hii leo; mambo ya hospital ya St Lukes na Mungu akitujalia, hii itakuwa hospitali bora na itashindana na Hospitali ya Rufaa ya Kilifi na hospitali nyinginezo inshallah," akasema Bw Mung'aro

## Kaunti yatoa chanjo ya mifugo kote Kilifi kupiga jeki ufugaji



Katika juhudi za kujitolea za kuipa umuhimu afya na ustawi wa mifugo, Serikali ya Kaunti ya Kilifi, kupitia Idara yake ya Mifugo, inazidi kutekeleza mpango wake mpana wa utoaji chanjo katika kaunti nzima.

Shughuli hiyo ya utoaji chanjo inanuia kufika kila pembe ya Kaunti ya Kilifi, ikilenga maeneo ya mbali na jamii zilizo hatarini zinazotegemea pakubwa ufugaji. Mbinu ya kimakinifu ya serikali ya kaunti inaakisi kujitolea kwake katika maslahi ya wanyama, utoshelevu wa chakula, na uwezeshaji wa wafugaji kiuchumi.

Kwa ushirikiano na maono ya pamoja, Serikali ya Kaunti ya Kilifi imejitolea kulinda mifugo, kudumisha kilimo endelevu, na kuinua maisha ya wafugaji. Shughuli hii ya chanjo inaashiria hatua muhimu katika kuhakikisha afya na ustawi wa wanyama katika Kaunti ya Kilifi, inayofungua fursa ya mustakabali mzuri katika sekta ya kilimo

## Tiba ya mfumo wa figo na fistula yaanzishwa hospitalini hapa



MHE Gideon Maitha Mung'aro alikagua kitengo kipya cha tiba ya mfumo wa figo chenye vitanda 3 katika hospitali hiyo. Kitengo hiki kinajumuisha kituo cha wauguzi na chumba cha kubadilishia mavazi, hiyo ikiashiria hatua muhimu katika ukwezaji wa hadhi ya hospitali hiyo hadi kuwa kituo cha afya cha Level V.

Tunayo furaha kutangaza kwamba Dkt Fernandes, mtaalamu wa magonjwa ya figo kutoka Cuba, atakuwa akifanya kazi katika kitengo hicho kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa. Zaidi ya hayo, upasuaji wa kutibu tatizo la Arteriovenous Fistula utafanywa na Dkt Nigel Amolo, ambaye ni mahiri wa upasuaji wa moyo na mishipa anayestakimu katika hospitali hiyo.

Ili kuhakikisha kuna upatikanaji wa huduma, NHIF itagharimia tiba ya mfumo wa figo. Tunahimiza sana kila mtu kujiandikisha na NHIF ili kunufaika kikamilifu na manufaa ya kitengo hicho.

## Mpango wa kutoa damu kwa wingi wazinduliwa




Mapema leo katika lango la Chuo Kikuu cha Pwani kwa ushirikiano na kikundi cha Kilifi Ultimate Bikers, nimezindua shindano la mbio za baiskeli kwa watu wazima na watoto wasiozidi umri wa miaka 14, ili kuhamasisha umma kuchangia damu kwa hiari.

Kampeni hii ya ukusanyaji wa damu kwa wingi ni juhudi za kukabiliana na hitaji kubwa la damu ya dharura katika Hospitali zetu na kupunguza mahangaiko kwa jamii za wagonjwa wanapokuwa na mgonjwa anayehitaji damu.

Hivi karibuni, Serikali yangu itazindua rasmi hifadhi ya damu katika Hospitali ndogo ya Malindi na tutaitekeleza shughuli ya utoaji wa damu kwa wingi angalau mara mbili kwa mwaka, ili Hospitali zetu ziweze kujitegemea katika suala la uhitaji wa damu. Damu ni zawadi ya uhai, tuchangie damu kwa wingi ili tuokoe maisha ya wengine.

Nation Media Group "Library Copy"

# DARUBINI KWA KAUNTI YA KILIFI

## Sherehe kubwa Gavana akizindua WiFi ya bure katika maeneo mbalimbali ya umma katika Kaunti



Vifijo na nderemo vilitanda huku Gavana wa Kaunti ya Kilifi, MHE. Gideon Mung'aro akizindua intaneti ya bure ya WiFi katika maeneo matano ya umma katika kaunti hii. Hafla ya uzinduzi huo iliyohudhuriwa na viongozi na wakazi wa Kaunti ya Kilifi wakiwemo Waziri wa Kaunti (CECM) anayesimamia Elimu na ICT, Mhe. Clara Chonga, ilifanyika katika Bustani ya Park. Maeneo mengine ambapo WiFi ya bure iliwekwa ni Soko la Ole Tiptip, Soko la Kwa Charo wa Mae, na Kituo cha Mabasi cha Kilifi.

Waziri Chonga pia alisisitiza umuhimu na usalama wa intaneti, na kuwahakikishia watumiaji kuwa ni salama kwa watu wa marika yote. Serikali ya Kaunti ya Kilifi, kupitia kwa Idara ya ICT, imejitolea sabili kuhakikisha kuwa raia wetu wote wanapata intaneti.

Katika hafla tofauti, Naibu Gavana Mhe. Flora Chibule aliongoza uzinduzi wa WiFi ya bure katika bustani ya Malindi Buntwani Waterfront. Kuzinduliwa huko kwa WiFi ya bure katika maeneo ya umma kote katika Kaunti ya Kilifi ni hatua muhimu kwa azimio la ujumuishaji wa kidijitali na ustawi wa kiuchumi. Hatua hiyo inatarajiwa kutoa fursa mpya kwa wakazi na wageni wanaotembelea kaunti hiyo, kukuza ubunifu na ujasiriamali.

## Ni afueni kwa wenye matatizo ya macho baada ya Kaunti kuanza kupeleka huduma hadi vijijini

Mariam Iha, mama wa miaka 67 kutoka eneo la Madzimbani, Wadi ya Mariakani, hakuamini alipoweza kuwaona vitukuu wake wanne kwa mara ya kwanza baada ya kufanyiwa upasuaji wa kuondoa utando katika macho yake. Aliponywa upofu.



Mariam aliyekuwa ameugua upofu uliotokana na utando kwenye lenzi za macho, kwa miaka 12, sasa ataweza kutazamana uso kwa macho na wajukuu wake 26.

Anamshukuru Mungu kwa kumwelekeza katika kambi ya macho ya Kaloleni Eye Inreach, ambayo ni mpango wa Kitengo cha Huduma za Macho cha Kaunti katika Hospitali ya Rufaa ya Kilifi

Uhamishaji wa huduma za macho hadi katika kila kaunti-ndogo kupitia mpango wa kila mwezi wa kuingia mashinani, ni ithibati tosha ya azimio la utawala wa Mhe Gideon Maitha Mung'aro la kufanikisha upatikanaji wa huduma nafuu za afya katika kila upembe wa Kaunti ya Kilifi.

## Amerika yarejeshea Kaunti vifaa vya kitamaduni/sanamu

Katika tukio la kipekee la kurejesha sanamu/vifaa vyetu vya kitamaduni, maafisa kutoka makavazi matatu na vyuo vikuu vya Marekani, ambayo ni The Denver Museum of Nature and Science, Illinois State Museum na Indianapolis Museum of Art, walitambua na kurejesha rasmi vifaa 85 vya kitamaduni vinavyojulikana kama Vigango kwa Jamii ya Mijikenda.

Tukio hili muhimu lilifanyika kwa ushirikiano na Makavazi ya Kitaifa ya Kenya na Idara ya Utamaduni na Turathi katika eneo la Kaya Kauma, pamoja na wadau mbalimbali muhimu wakijumuisha shirika la UNESCO, Tume ya Kitaifa ya UNESCO ya Kenya (KNATCOM), na WESLUX.

Hafla ya kukabidhi vifaa hivyo vya kale kwa wenyeji ilihudhuriwa na watu mashuhuri kama vile Mhe. Peninah Malonza aliye Waziri wa Utalii, Wanyamapori na Turathi, Mhe. Salim Mvurya aliye Waziri wa Madini, Uchumi wa Baharini, na Shughuli za Baharini, Bi Ummi Bashir aliye Katibu wa Idara ya Utamaduni na Turathi, Mhe Gavana Gideon Maitha Mung'aro, Afisa Mkuu Dkt Ruth Dama Masha akiandamana na Waziri wa Elimu na ICT, Mhe. Clara Chonga pamoja na maafisa wengine wa serikali ya Kaunti na Kitaifa.

Vigango, vilivyo na kimo cha futi saba kila kimoja, vilisimikwa kitamaduni mbele ya nyumba kadhaa kuwakumbuka wakongwe mashuhuri wa kiume waliofariki katika jamii ya Mijikenda. Jamii hii inazichukulia sanamu hizi kwa heshima kubwa. Inaamini, aghalabu kuwa, maafa kama vile magonjwa, ukame, na mazao duni yanatokana na kukosekana kwa sanamu hizo. Waziri Malonza alisisitiza umuhimu wa sanamu hizo kwa jamii za Pwani na athari mbaya zinazosababishwa na wizi wa vifaa hivyo, akihimiza kurudishwa kwavyo 'nyumbani' Kenya.

Tukio hili la kipekee la kurejeshwa nyumbani kwa vifaa hivyo, ni mfano wa azimio la kimataifa la kurekebisha dhuluma za kijadi, kutambua turathi za kitamaduni, na kulinda uhusiano mtakatifu kati ya jamii na vitu vyao vya kisanii.



## Hospitali yapata wataalamu wa matibabu ya dharura pamoja na madereva wa ambulensi

Tuna furaha kutangaza kuwasili kwa matabibu wa dharura na madereva wa ambulensi wenye ujuzi ambao wataimarisha utoaji wa huduma mbalimbali za matibabu ya dharura katika kaunti hii.



Ili kuadhimisha hafla hii, sherehe ya kusaini mkataba wa wataalamu wapya wa EMT, ukiongozwa na MHE. Felkin Kaingu, Waziri wa Kaunti (CECM) anayesimamia Utumishi wa Umma, Dkt David Mulewa, Afisa Mkuu wa Afya na Usafi wa Mazingira na Eliud Kalama, Afisa Mkuu wa Usimamizi wa Utumishi wa Umma.

Hafla hiyo ilitoa mafunzo muhimu kuhusu masuala mbalimbali, zikiwemo kanuni za maadili kwa watumishi wa umma, huduma bora kwa wateja, maadili ya kazi, huduma na mawasiliano kwa wagonjwa, uwekaji kumbukumbu na kujilinda.

Mpango huu unaashiria hatua muhimu kwa serikali ya kaunti ya Kilifi kuwapa raia wake haki yao ya afya.

## Uzinduzi wa Hazina ya WezeshaFunda kwa Ushirikiano na Benki za Rafiki Microfinance, KCB na Kaunti ya Kilifi



Hazina hii iliyobuniwa upya itasaidia sana kukuza biashara ndogo ndogo (SMEs)

Hazina ya Wezesha imejikita katika Sheria ya Mikopo Midogo ya Kaunti ya Kilifi (2016). Hivi karibuni sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho ya tatu ya kubadilisha jina kutoka Hazina ya Mbegu na kuwa Hazina ya Wezesha.

Hazina hii pia imekumbatia mabadiliko mengine mawili makubwa. Kwanza, hazina hiyo sasa imegatuliwa zaidi hadi kiwango cha wadi, ili kuwawezesha wanaonufaika kutuma maombi katika wadi zao na sio katika kaunti ndogo. Zaidi ya hayo, sasa tuna mpango kwa Serikali ya Kaunti ya Kilifi kushirikiana na taasisi za kifedha kwa usimamizi wa hazina.

Hazina hiyo imeshirikiana na Benki ya Kenya Commercial na Benki ya Rafiki Microfinance ili kuifanya kuwa imara zaidi katika kukidhi mahitaji ya watu wa Kilifi.

Sasa tumetenga Sh200 milioni kwa Mwaka wa Kifedha wa 2023/2024 kutoko Sh116m za awali. Kwa ushirikiano wa taasisi za kifedha, tutakuwa na uwezo wa kutoa mkopo hadi Sh1 bilioni kwani zitalingana na kila shilingi na shilingi tano.

Tumehakikisha kwamba mikopo hiyo haina riba kabisa na inatii Sheria, huku wanaonufaika wakilipa 4% tu ya ada ya usimamizi.

## Tiba ya upasuaji wa uti wa mgongo na mishipa yafaulu

Ungana nasi kuipongeza Hospitali ya Kaunti-ndogo ya Mariakani kwa kufanikisha upasuaji wa kwanza kabisa wa uti wa mgongo hapo jana. Mafanikio haya ya kipekee yanaashiria hatua muhimu kwa mhazigi (daktari wa upasuaji wa mifupa na misuli), Dkt Mustafa Khanbai na kikosi chake kilichojitolea.



Serikali ya Kaunti ya Kilifi itaendelea kujitolea kutoa huduma maalumu za matibabu katika kila pembe ya Kaunti, kulingana na maazimio ya MHE. Gideon Maitha Mung'aro.

Nation Media Group "Library Copy"
Nation Media Group "Library Copy"
Nation Media Group "Library Copy"